# HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU

*(Barua zote za kiofisi zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)*

**Mkoa wa Arusha**
**Telegram: Meru**
**Simu: (+ 255) 027 254-1112**
**Faksi: (+ 255) 027 254-1112**
**Barua pepe:merudc@yahoo.com**
***Tovuti : www.merudc.ao.tz***

Ukumbi wa Wilaya,
S.L.P 462,
**USA RIVER**

**23.06.2020**

## TANGAZO LA ZABUNI

Halmashauri ya Wilaya ya Meru inawatangazia zabuni wananchi wote wenye uwezo na sifa ya kukusanya ushuru/mapato ya Halmashauri na usafishaji wa mazingirakwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021kama ifuatavyo:

**(A) UWAKALA WA KUKUSANYA MAPATO:**

| NA. | AINA YA ZABUNI | NAMBA YA ZABUNI | ENEO LA KUKUSANYA USHURU TARAFA/KATA |
|---|---|---|---|
| 1. | USHURU WA MAZAO | LGA/001/2020/2021/NC /57/01 | KATA ZA - NGARENANYUKI, NGABOBO NA UWIRO |
| 2. | USHURU WA MAZAO | LGA/001/2020/2021/NC /56/02 | KATA ZA - AKHERI,SONGORO NA NKOARISAMBU |
| 3. | USHURU WA MAZAO | LGA/001/2020/2021/NC /58/03 | KATA ZA -MARORONI NA KIKATITI |
| 4. | USHURU WA MAZAO | LGA/001/2020/2021/ NC/40/04 | KATA ZA - KIKWE NA MBUGUNI |

**(B) UWAKALA WA USAFISHAJI WA MAZINGIRA:**

| NA. | AINA YA ZABUNI | NAMBA YA ZABUNI | ENEO LA USAFISHAJI |
|---|---|---|---|
| 1. | Usafishaji wa mazingira | LGA/001/2020/2021/NC /55/05 | Kata za **Ambureni, Akheri, Sing'isi Na Poli na usafi katika soko la Tengeru na Msorongo (**Usafi katika soko la Tengeru na Msorongo ni pamoja na kufagia soko na kuzoa taka kwenda dampo kuu la Halmashauri) Kuondoa taka zote katika masoko mengine eneo la kazi. |
| 2. | Usafishaji wa mazingira | LGA/001/2020/2021/NC /55/06 | **Mamlaka Ya Mji Mdogo Usa River,Kata yaNkoaranga***(Kijiji cha Nshupu, Pia Kata ya***Nkoanekoli** *Kitongoji cha Mangusha*) na Usimamizi na usukumaji taka katika **Dampo la muda la Maroroni (**Usimamizi maana yake ni kuhakikisha hakunamtu yeyote anatupa taka nje ya shimo wala barabarani, kusukuma taka ndani ya shimo kwa kutumia mtambo(bulldozer) pindi likijaa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | ama kuziba njia kwa ajili ya kuwezesha magari ya taka kumwaga taka na kugeuka katika kipindi chote cha muda wa zabuni, kupiga sumu ya kuuwa wadudu kama inzi na harufu, kuweka udongo juu ya taka kila siku ya jumamosi ya kila wiki). |
| 3. | Usafishaji wa mazingira | LGA/001/2020/2021/NC /55/07 | Kata ya **Imbaseni, Maji Ya Chai, Kikatiti, na Malula** (fungu hili litajumuisha pia kufagia na kuzoa taka zote katika masoko kikatiti na kolila). |

**MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI**

**Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo:-**

1. Mwombaji lazima awe na leseni hai na stahili ya biashara(Certificate of Registration na Extract), Hati ya Usajili wa jina la biashara na ofisi inayotambulika.

2. Mwombaji awe na uwezo wa kifedha, athibitishe kwa kuambatanisha 'Bank Statement' ya miezi mitatu (3) iliyopita kutoka tarehe aliyoomba zabuni au 'Audited Financial Statement'ya miaka mitatu ya karibuni.

3. Mwombaji aambatanishe "Power of Attorney" kwa zabuni husika.Bid

4. Mwombaji aambatanishe TAMKO RASMI LA VITENDO DHIDI YA KUZUIA RUSHWA iliyosainiwa na mwombaji mwenyewe,Power of attorney, Uthibitisho wa Uthibitisho wa Mlipa kodi (Tax Clearance),Maoteo na Taarifa kamili ya Mzabuni.

5. Mwombaji awe na vifaa vya kutosha kumudu vyema zabuni aliyoomba.

6. Mwombajiawetayari kulipa dhamana ya zabuniya kiwango cha miezimitatu (3) cha maoteo kwa mwezi na awe na wadhamini wawili wenye mali zisizohamishika na wanaotambulika, kabla ya kusaini mkataba.

7. Awe tayari kutumia viwango vilivyowekwa katika Sheria ndogo za Halmashaurivya ukusanyaji wa mapato.

8. Mzabuni atakayeteuliwa atatumia mashine za kielektroniki (POS) kukusanyia ushuru wa Halmashauri.Bid validity period ni siku 90.

9. Maombi yatakayoletwa kwa njia ya Fax, Telefax, na Telegraphic System na yatakayochelewa hayatapokelewa na hayatafunguliwa siku ya ufunguzi.

10. Vikundi vya Kijamii (CBOs) ziambatanishe orodha ya viongozi wa kikundi na barua za utambulisho kutoka katika kata husika.

11. Mwombaji awe na magari yenye hali nzuri kwa kusafirishia taka kwenda dampo, Vifaa vya kutosha kusafishia, wafanyakazi/vibarua wa kutosha kutokana na ukubwa wa eneo analoomba, pamoja na ofisi ya kudumu.

12. Mwombaji asiwe na deni lolote analodaiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Aidha, mwombaji aliyewahi kushitakiana na Halmashauri ya Wilaya ya Meru kuhusiana na kazi yeyote, hatapewa nafasi ya ushindani kwa kazi yeyote ya zabuni iliyotangazwa na Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Vile vile mawakala watakaothibitika kuwa na tuhuma za utendaji usiozingatia Sheria kutoka taasisi nyingine za Serikali hawatapewa nafasi ya ushindani kwa kazi zinazotangazwa na Halmashauri ya Wilaya ya Meru.

13. Kabrasha la zabuni na maelezo mengine yanapatikana katika Mtandao wa **TANEPS** kupitia tovuti ya www.taneps.go.tz. Kwa maelezo zaidi tembelea ofisi za Makao makuu ya Halmashauri ya Meru, Usa River, katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni, Chumba Na.36, Ghorofa ya kwanza, kuanzia saa 1:30 asubuhi mpaka saa 9:30 alasiri (siku za Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu za kitaifa)

14. Maombi ya Zabuni zote yawasilishwe kwa njia ya TANEPS. Mwisho wa kupokea maombi hayo ni ***Jumatatu, tarehe 06/07/2020, saa nne (4) asubuhi***. Waombaji wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni hizo kwa kupitia mfumo wa TANEPS ( Tanzania National e-Procurement System) utakaofanyika siku hiyo ya tarehe ***06/07/2020 saa nne (4) asubuhi*** katika mfumo wa TANEPS.

Emmanuel J. Mkongo
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA MERU**

MKURUGEZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU
S.L.P. 462 USA RIVER
MERU - ARUSHA